Mungu Aliumba Wanyama

(God Made Animals)

Na Eric Lyons

Kimetafsiriwa kwa Kiswahili na Xavery Ngullo

(Translated into Swahili by …)

Kitabu kimehaririwa na: T.L.G. Raynor

(Edited by …)

Page 1 (note to parents)

Kwa Wazazi

Waandikaji wa Utetezi (Apologetics Press), ni shirika lisilo la biashara limejitolea kwa ajili ya utetezi wa Ukristo wa Agano Jipya. Kwa zaidi ya robo-karne tumetengeneza vitu vingi vya kujenga imani ya watu wazima. Na tumezalisha vitu vingi kama vile Ugunduzi (Discovery), Safu za Mtafiti (Explorer), na baadhi ya vitabu kwa ajili ya vijana wa daraja la tatu shule za sekondari. Na sasa tumependezwa kutoa safu mpya ya vitabu hata kwa watoto wadogo zaidi.

Shirika la "Apologetics Press Early Reader Series" (Waandishi wa Utetezi kwa Safu ya Mwanzo ya Msomaji) ni vitabu vilivyolengwa kwa watoto katika shule za chekechea, mpaka darasa la pili. Inategemea umri wa watoto wako, safu hii inaweza kumwezesha mzazi kuchagua kuwasomea watoto wao, au kusoma pamoja na watoto wao au kusikiliza wanaposoma watoto wao, wanaposoma kwa sauti kubwa.

Vitabu vya safu hii vimejaa picha za rangi mzuri na dhahiri na habari nzuri kuhusu Mungu, Viumbe Vyake, na neno Lake. Vitabu hivi vimeandikwa kwa kiwango ambacho wasomaji wapya watakifurahia, na hilo litawavutia kwa Muumbaji wao.

Tunategemea kuwa mtaifurahia kutumia safu hii ya Waandishi wa safu za Mwanzo za Msomaji kuwafundishia watoto wenu, kusoma, kwa wakati huo huo wakijifunza kuhusu Mungu na viumbe Vyake.

Page 2 ***(book information)***

Mungu Aliumba Ulimwengu
Na Eric Lyons
Kimeandikwa (Copyright ©) 2005
Apologetics Press
Haki zote zimehifadhiwa.
Hakuna ruhusa ya kunukuu sehemu ya kitabu hiki kwa namaa yoyote bila kibali cha mhariri wa kitabu.
ISBN: 0-932859-70-4
Maktaba ya Congress: 2005926996
Kimepigwa chapa nchini China.

Page 3 (title)

Mungu Aliumba Wanyama

Na Eric Lyons

Page 4
Wanyama na wanadamu wamekuwa wakiishi pamoja tangu siku ya sita ya uumbaji.

Page 5
Tangu wakati wa adamu na hawa, wanaume kwa wanawake wamejifunza viumbe wa Mungu waliowaajabu. Tumejifunza mengi sana kuhusu wao.

(sign on the boat at the bottom of the page)
Karibu Maesa kambi ya tembo!

Page 6
Mungu aliumba tembo akiwa na mwili mkubwa pamoja na mkonga mrefu. Tembo wengine hukua na kuwa na uzito mkubwa kuliko basi la shule.

Page 7
Paka-mwitu ni paka wakubwa sana waishio mwituni. Wanao uwezo wa kuruka kiasi cha futi 18 kuenda juu. Hiyo ni karibu mara mbili ya urefu wa goli la mpira wa kikapu.

Page 8
Mungu alibuni ngamia wakiwa na nundu migongoni mwao. Baadhi ya ngamia wanayo nundu moja tu. Wengine wanazo nundu mbili.

Page 9
Ngamia huhifadhi mafuta katika nundu zao. Wanapokuwa na safari bila chakula kwa muda mrefu miili yao hutumia mafuta haya kwa chakula. Ngamia wanao uwezo wa kuenda mwendo wa juma (na zaidi) bila kunywa maji.

Page 10
Miguu ya ota iliyobetuka na mkia wake mrefu humfanya awe mwogeleaji mashuhuri.

Page 11
Korongo ni ndege wa rangi ya waridi wenye miguu mirefu. Utawaona mara nyingi nedege hawa wakisimamia mguu mmoja wanapokula na wanapolala.

Page 12
Duma ndiye mnyama mwenye mwendo mkali kuliko wote wa nchi kavu. Ana mwendo mkali kuliko baadhi ya mageri!

Page 13
Mbuni ni ndege mkubwa zaidi duniani. Tofauti na ndege wengine, mbuni hawezi kupaa angani. Lakini anauwezo wa kukimbia haraka.

Page 14
Penqwini ni aina nyingine yandege ambaye hawawezi kuruka anagani. Pengwini wengi wao huishi sehemu za baridi sana.

Page 15
Farasi wa baharini ana kichwa ambacho kimefanana na kichwa cha farasi.
Farasi wa baharini hubadilika rangi wakati hatari inapokaribia.

Page 16
Kasa (kobe) ni baadhi ya wanyama watembeao taratibu sana duniani.
Mungu alibuni gamba gumu ambalo huwakinga wasiliwe na wanyama wengine.

Page 17
Mnyama mmoja ambaye anatembea polepole kuliko kasa anaitwa slothi. Huwa inamchukua slothi saa nzima kutembea umbali wa uwanja wa mpila.

Page 19
Mnyama mkubwa kuliko wote ni nyangumi wa bluu ee ni mkubwa kuliko dinosoria yeyote aliyewahi kupatikana.
Nyangumi wa bluu ana moyo mkubwa kama gari ndogo.

Page 20
Nyani wanafurahisha kuwatazama.
Kama muonavyo Mungu aliumba nyani tofauti na wewe, ulivyo.

Page 21
Mungu aliumba kangaruu wakiwa na mifuko maalumu ambayo kangaruu wadogo huishi. Watoto wa kangaruu huitwa joey.

Page 22
Dubu panda hutumia kiasi cha saa 12 kula mianzi kwa kila siku. Anakula chakula kingi zaidi kwa siku moja kuliko unachokula wewe kwa juma zima.

Page 23
Simba ni mfalme wa msituni wala hakuna kinachomtisha.

Page 24
Mdomo wa kinyama-ndege ulibuniwa vizuri kwaajili ya kukusanya vyakula kutoka chini ya mito.

Page 25
Chatu hutumia sauti yao kutoa kishindo cha onyo wanapohisi kwamba hatari imekaribia.

Page 26
Cheche ni baadhi ya wanyama wenye harufu mbaya duniani. Mungu aliwapa uwezo wa kuwwaga maji maji yenye harufu mbaya sana kutoka chini ya mikia yao wanapotishiwa.

Page 27
Dubu wa kizioni wanaishi sehemu za baridi sana.
Mungu aliwaumba wanyama hawa na uwezo mzuri sana wa kunusa.

Page 28
Mungu alifanya aina nyingi za papa.
Kuna wengine ni wakubwa kuliko gari.
Wengine ni wadogo kiasi cha kutosha kwenye sanduku la vifaa.

Page 29
Ni nani aliyeumba papa kuwa waogeleaji wazuri hivi?

Page 30
Twiga ndio wanyama warefu zaidi duniani.
Shingo zao ndefu huwasaidia kupata chakula ambacho wanyama wengine hawakifikii.

Page 31
Mungu alimfanya gogota akiwa na uwezo wa kutoboa shina la mti bila kuumiza kichwa chake.

Page 32
Mungu aliumba wanyama wote hawa wazuri. Je, na wewe umemshukuru Mungu leo kwa uumbaji Wake mzuri?

Back Page

Tunaanzisha A.P. Reader Series *(Introducing…)*

Tangu siku ya tano na ya sita ya uumbaji, wanyama wameishi hapa duniani kama ushuhuda wa kuwepo kwa Mungu. Kadiri tunavyozidi kujifunza kuhusu Mungu, ndivyo tunavyozidi kushangazwa na Yule Aliyeviumba uwezo wa duma wa kukimbia, mkonga wa tembo, harufu ya vicheche, gamba la kasa (kobe) vyote vinatuelekeza kuhusu kuwepo Muumbaji. Katika hii A.P. Msomaji, nao watashangazwa na viumbe wengi ambao Mungu aliwaumba.

Kuhusu A.P. Safu ya Wasomaji ***(About the A.P. Reader Series)***

Kuna njia gani nyingine iliyobora ya kujifunzia kusoma kuliko kuanza kwa kusoma kuhusu Mungu na Uumbaji wake? Siyo tu kwamba watoto wenu watasoma kuhusu anga, miti, pamoja na wadudu, bali pia watajifunza kuhusiana na Mbunifu aliyefanya mambo hayo yote kwa maandishi ya kueleweka, picha, watoto wenu watapenda kusoma na pia Watampenda Muumbaji wao.